**SALAMU MAALUMU KUTOKA KWA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI YA MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA, WAKATI WA KUSHEREHEKEA SIKU YA AFYA YA MIMEA KIMATAIFA, INAYOFANYIKA ARUSHA LEO TAREHE 12 MEI, 2024, PROF ANDREW EPHRAIM TEMU**

- **Mgeni Rasmi, Mheshimiwa Hilda Kinanga, Mkurugenzi, Utawala na Rasilimali,** Mwakilishi wa Katibu Mkuu, **Wizara ya Kilimo;**
- **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Ndugu Paul Makonda.**
- **Mwakilishi Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO); Mr. Monday.**
- **Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania – Prof. Joseph Ndunguru;**
- **Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TPHPA;**
- **Wadau wa Afya ya Mimea;**
- **Menejimenti na watumishi wote wa TPHPA;**
- **Waandishi wa Habari;**
- **Wananchi wa Mkoa wa Arusha na wale Mliosafiri kushiriki leo;**
- **Wageni waalikwa;**

**Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana,**

Napenda kumshukuru Mwenyezi **MUNGU** kwa kutuwezesha kukutana hapa Arusha leo kusherehekea siku ya Afya ya Mimea Duniani, Tarehe 12 May Mwaka 2024.

Kauli mbiu yetu leo ni **"Afya ya Mimea, Biashara Salama na Teknolojia za Kidijiti"** ikilenga umuhimu wa matumizi ya tekinolojia za kidigiti katika kulinda Afya ya Mimea, Biashara Salama, na Rasilimali zetu za mimea.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana, Wageni waalikwa,**

Kwa kuadhimisha Siku ya Afya ya Mimea Duniani tunadhihirisha tunatambua jukumu lisiloepukika la mimea katika kudumisha uhai katika sayari yetu.

Leo, tunaenzi uhai wa mimea na tanaelimishana na kuhamasishana katika kukabiliana na changamoto ambazo mimea inazikabili wakati huu wa mabadiliko ya sekta ya kilimo na hali ya hewa. Kilimo kinatambulika kuwa kati ya nguzo kuu ya uchumi wetu hapa Tanzania.

**Mheshimiwa mgeni rasmi,**

Bodi ya TPHPA inatambua na kuyaishi matokeo ya juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita na ya Wizara ya Kilimo katika sekta. Ukuaji wa bajeti ya kilimo ni jambo la wazi, tunaelekea kutimiza malengo ya Azimio la Malabo la mwaka 2014 juu ya kukuza kilimo na kuboresha Maisha ya watu wengi.

Sasa tunashuhudia bajeti ya zaidi ya Trilioni 1.2, jambo ambalo miaka kadhaa ya nyuma halikuwezekana.

Na si bajeti tu, msukumo mkubwa kwenye sekta ya kilimo, uwezeshaji wa vijana kuingia kwenye kilimo, uwekezaji wa sekta binafsi katika mnyororo mzima wa thamani wa bidhaa za kilimo ni mambo yanayotia moyo sana.

Msisitizo unaowekwa wa usimamizi wa masuala ya kilimo katika ngazi za Wilaya, Halmashauri na Mikoa, ushiriki wa Mashirika yasio ya Kiserekali na wadau wa maendeleo ya kimataifa kwa mfano Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Cahkula Duniani (FAO) na mengine, vyote vinapelekea ongezeko la rasilimali za sekta, heshima stahili kwa wakulima, kutambulika kwa mchango wa watoa huduma kwenye sekta na wasindikaji wa mazao, ongezeko la tija na kuongezeka kwa uzalishaji. Mifumo mipya ya kufikia masoko hususan TMX, stakabadhi ghalani na minada tofauti, vyote vimenyanyua maendeleo ya kilimo na kuleta tija ya juu zaidi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** matokeo ya juhudi zote hizi yanadhihirika ifuatavyo:

- *Maeneo ya uzalishaji kwa hekta yanaongezeka aghalabu kwa kasi tofauti kulingana na aina ya zao.*
- *Kilimo cha umwagiliaji kimekuwa kwa kasi na sasa ni hekta 983,466.*
- *Mwaka 2023 sekta imekua kwa asilimia 4.2 (3.3 mwaka 2022)*
- *Sekta imechangia asilimia 26.5 ya pato la taifa (26.2 mwaka 2022)*
- *Imezalisha asilimia 65 ya malighafi za viwanda vyetu.*
- *Mauzo nje ya nchi mwaka 2022/2023 ni* ***Dola za Kimarekani Bn 2.3 (1.2 - 2019/20)***
- *Sekta imeendelkea kuhakikisha usalama wa chakula.*

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Bodi ya TPHPA inauangalia ukuaji huu wa uzalishaji na wa biashara ya mazao kilimo nje ya nchi kwa makini. Pamoja na faida zake, pia unaashiria changamoto mpya katika tasnia ya afya ya mimea. Bodi ya TPHPA inajipanga ile iweze kuona mbele na kubuni mikakati ya kukabiliana na hali hiyo.

Ongezeko la ekari zinazolimwa, matumizi makubwa zaidi ya mbolea za kisasa, mahitaji na matumizi makubwa zaidi ya viuatilifu *(sumu za kuangamiza wadudu na kutibu magonjwa)*, kukua kwa biashara ya nje na hivyo muingiliano mkubwa zaidi

wa watu na bidhaa kwenye mipaka yetu, vyote vitapelekea changamoto kubwa zaidi na za aina tofauti katika kusimamia afya ya mimea na usafi wa mazao tuuzayo nje.

Milipuko kama ya viwavi jeshi, ya ndege wavamizi kama kwelea kwelea, nzige na kadhalika, wanaweza kushamiri zaidi kadri tunavyopanua mashamba yetu na kufungua mapya. Changamoto hii inakuwa kubwa zaidi kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Kwa kuelewa hivyo, Bodi ya Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu inajipanga kuiongoza Mamlaka kuwa tayari kulinda mafanikio tunayoyapata kutokana na uwekezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Naomba nitumie fursa hii ya siku ya afya ya mimea, kuainisha changamoto kadhaa ambazo Bodi inaziona mbele yetu na namna ambavyo tumekwisha anza kuiongoza manejimenti kukabiliana nazo.

**CHANGAMOTO ZINAZOTAMBULIWA NA BODI**

1. **Kuibuka kwa Vidudu na Magonjwa Mapya** *(Emerging Pests and Diseases):* Hii ni hali ambapo wadudu na magonjwa mapya yanajitokeza kuwa na athari kubwa kwa afya ya mimea.
2. **Kuwepo na Spishi Vamizi (**Invasive *Species***):*** Hizi ni spishi za mimea ambazo zinaingilia mfumo wa ekolojia asilia na kushindana na mimea mingine na kushusha tija.
3. **Mabadiliko ya Hali ya Hewa** (*Climate change*): Haya ni mabadiliko katika mifumo ya hali ya hewa. Haswa joto, unyevu kwenye udongo na hewa, na viwango vya mvua. Mabadiliko haya yanaweza kusababisha kuongezeka kwa magonjwa na wadudu, kupunguza ufanisi wa viuatilifu, ufanisi wa mbinu mbadala kama IPM, na hivyo kuathiri wingi na ubora mavuno.
4. **Usugu wa Dawa za Kuulia Wadudu** *(Pesticide Resistance)*: Hii ni hali ambapo wadudu wanakuwa na uwezo wa kustahimili athari za viuatilifu kutokana na mabadiliko kimazingira au matumizi yasiyo sahihi ya sumu hizo.
5. **Kupotea kwa Jeni Tofauti** (*Loss of Genetic Diversity*): Wanasayansi wanatumabia hii ni hali ambapo kuna kupotea au kupungua kwa utofauti wa jenetiki katika mimea ya kilimo na spishi za asili. Hii husababisha kupungua kwa uwezo wa mimea kukabiliana na vihatarishi.
6. **Biashara ya Kimataifa na Usalama wa Kibaiolojia** (*Global Trade and Biosecurity*) : Hapa tunaongelea mifumo ya biashara ya kimataifa ambayo inahusisha usafirishaji wa bidhaa za mimea na viumbehai. Mifumo ikibadilika huleta changamoto mpya na hatari za kuingiza wadudu na magonjwa nchini.

Vile vile tunaweza kupoteza masoko kwenye nchi ambazo zimepiga marufuku mazao yenye madhara fulani.

7. **Kudorora kwa Afya ya Mimea bila Visumbufu vya Kibailojia** *(Abiotic Plant Health Challenges)*. Hapa tunaongelea kudorora kwa afya ya mimea pasipo mashambulizi ya kibailojia. Visababishi vinaweza kuwa ni mabadiliko ya hali ya hewa, lishe mbaya ya mimea, mimea shindani, matumizi mabaya ya mbegu, ushauri wa kilimo usiokidhi vigezo, nk.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Nimalizie kwa kuainisha mwelekeo wa Bodi katika kubabiliana na changamoto hizi. Kwa mamlaka ambayo Bodi imepewa na Sheria Namba 4 ya Mwaka 2020, na Kanuni na Miongozo za mwaka 2022, Bodi itaendelea na majukumu yake yalioainishwa humo na kuweka msisitizo wa ziada kwenye mambo yafuatayo:

1. **Kuhakikisha TPHPA inatekeleza Majukumu yake Kama NPPO**: Bodi itaendelea kuongoza juhudi za kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa afya ya mimea na kulinda afya ya mimea kwa kuheshimu Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Mimea (IPPC).

2. **Uimarishaji wa Uwezo wa Mamlaka:** Bodi itaendelea kuweka kipaumbele katika kuimarisha rasilimali watu na vitendea kazi, mahusiano na wadau tunaoshirikiana nao katika kutekeleza majukumu yetu ya kugundua na kuzuia vihatarishi, wadudu na magonjwa ya mimea.

3. **Kushabihisha Utafiti na Ubunifu:** Bodi itatoa muelekeo na msaada unaohitajika kwa Menejimenti katika kuhakikisha tunashirikiana na taasisi rasmi za utafiti hususan TARI, TOSCI, TACRI, ASA, TAHA na nyingine katika utafiti na ubunifu wa mbinu za usimamizi wa afya ya mimea.

   Bodi itaendelea kuitaka menejimenti kushirikiana na NPPOs za nchi nyingine na Wadau wa Maendeleo tulio na malengo yanayofanana. Kwa kipekee naomba nichukue fursa hii kutambua mashirika yafuatayo kwa ushurikiano na miongozo thabiti:

   *i.* **Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO):** *linaloongoza juhudi za kimataifa za kukabiliana na njaa ikiwa ni pamoja na afya ya mimea na usimamizi wa viuatilifu.*

   *ii.* **Umoja wa Nchi za Ulaya (EU).** *Mfuko wake wa maendeleo ni mfadhili mahiri wa miradi ya afya ya mimea.*

   iii. **Shirika la Afya Duniani (WHO):** *linalotoa uongozi wa kimataifa juu ya masuala ya afya, ikiwa ni pamoja na tathmini ya mabaki ya viuatilifu katika chakula na athari zake kwa afya ya binadamu.*

iv. **Shirika la Ulinzi wa Mazingira (EPA**): *inasimamia sumu za kuua wadudu na kuweka viwango vya matumizi yao salama kulinda afya ya binadamu na mazingira.*

v. **Mamlaka ya Usalama wa Chakula ya Ulaya (EFSA):** *Shirika la Umoja wa Ulaya linalohusika na kutathmini na kuwasiliana hatari zinazohusiana na mnyororo wa chakula, ikiwa ni pamoja na viuatilifu.*

vi. **Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Mimea (IPPC**): *Shirika la kiserikali linalolenga kulinda rasilimali za mimea kutokana na wadudu na magonjwa, na kuwezesha biashara salama ya kimataifa.*

vii. **CropLife International**: *Shirikisho la kimataifa linalowakilisha sekta ya sayansi ya mimea, ikiwa ni pamoja na wazalishaji wa dawa, ambayo inatetea mazoea endelevu ya kilimo na matumizi ya dawa ya kuwajibika.*

viii. **Mkaguzi wa Afya za Mimea Kenya** *(KEPHIS - Kenya Plant Health Inspectorate Services).*

ix. **Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa** (WHO- World Health Organization)

4. **Bodi itaendelea kuhimiza na kuwezesha mawasiliano na mawasilisho ya masuala ya Afya ya Mimea**: Bodi imeweka kipaumbele katika juhudi za mawasiliano na kuwafikia wadau wote ili kuwashirikisha katika usimamizi wa afya za mimea. Leo, siku ya Afya ya Mimea Duniani ni fursa nyingine ya kusambaza taarifa, uelewa na habari kuhusu changamoto za afya ya mimea, mipango bora, na umuhimu wa hatua za pamoja.

5. **Kusimamia ufuatiliaji na kutoa taarifa za Afya ya Mimea:** Bodi itaweka kipaumbele katika kusimika ***mifumo ya kidijitali ya ukusanyaji wa takwimu***, uchambuzi wake ikiwemo ***uchambuzi wa takwimu kubwa*** (***Big Data Analysis****)* ili kufanikisha kwa urahisi zaidi ugunduzi wa mapema na kutoa majibu ya haraka kwa vihatarishi vinavyojitokeza.

6. **Kusimamia Mbinu Himilivu katika Tasnia ya Afya ya Mimea na Matumizi ya Viuatilifu**: Bodi itaendelea kuhamasisha mbinu endelevu katika usimamizi wa afya ya mimea ambazo zinapunguza matumizi ya sumu na kikemikali, haswa sumu na kemikali zenye athari kubwa *(**highly hazardous pesticides**)*. Mbinu hizi zinajumuisha uhifadhi wa bioanuwai na kuongeza uimara wa mifumo ya kilimo **(*<u>Intergrated Pest Management</u>* <u>systems</u>)** pamoja na matumizi ya viuatilifu vya kibaiologia (***<u>Biological Pest Control</u>***).

7. **Kuhimiza Matumizi ya Akili Bandia**: Bodi itasisitiza elimu, ufahamu na matumizi ya akili bandia kwa mapana yake. Kuna mifano kadhaa ambayo inatoa mwelekeo na matamanio ya Bodi kwenye eneo hili:

    a. **Utabiri wa vihatarishi kwa kutumia mifumo bandia** (*<u>Predictive Modeling Applications</u>*),
    b. **Kuhimiza Kilimo cha Usahihi** *(<u>Precision Agriculture</u>)* kama njia ya kukabiliana na vishambulizi, vya kibaiotiki na visivyo, vya afya za mimea.

c. **Sayansi ya Jeni na Uzazi** *(Genomics and Breeding)* haswa kutumia algorithms za akili bandia kuchambua data za jeni na kutambua alama za jeni zinazohusiana na upinzani au uvumilivu wa magonjwa kwenye mazao.
d. **Kukusanya na kutumia Takwimu Kubwa katika Maamuzi** *(Big Data Analysis).* Kwa mfano - TPHPA inaweza kuunganisha vyanzo tofauti vya takwimu kama picha za satelaiti, takwimu za hali ya hewa, rekodi mbali mbali za sekta za uzalishaji katika sekta ya kilimo na kutumia mbinu za akili bandia kutoa ufahamu kamili na utabiri wa masuala ya afya ya mimea.

8. **Kuzitumia Maktaba na Benki ya Jeni za Mimea kuimarisha Afya ya Mimea**: Bodi itahimiza na kuendelea kuwekeza katika maktaba ya mimea *(**Herbarium**)* ili kuiwezesha kutoa huduma za utambuzi wa spishi mbali mbali, kufuatilia spishi zenye uvamizi, spishi zenye uwezo wa kudhibiti magonjwa na wadudu wa mimea, kuchangia katika uhifadhi utofauti wa jeni, na kuwezesha elimu, utafiti na ushirikiano ndani ya jamii ya kisayansi, Tanzania, Afrika na Ulimwenguni.

   Kwa upande wa **Benki za maumbile ya mimea** (*Gene Bank*), msisitizo utakuwa katika kutumika kama hazina ya utofauti wa maumbile (***Genetic Diversity***) ambazo ni muhimu kwa kuboresha afya ya mimea kupitia mipango ya kuzaliana (***plant breeding***).

Bodi ya Wakurugenzi, Afya ya Mimea na Viuatilifu inaamini kwa kuzingatia maeneo haya itachangia katika malengo endelevu yanayohusiana na usalama wa chakula, uhifadhi wa mazingira na ustawi wa kiuchumi.

Nimalize kwa kutoa Shukurani za dhati kwa:
- Serikali ya JMT inayoongozwa na ***Mh. Rais Dr. Samia Suluhu Hassan***,
- Wizara ya kilimo, ***Waziri Mh. Hussein Bashe***, ***Naibu Waziri Mh. Silinde***, ***Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watumishi*** wote Wizara ya Kilimo.
- **Msajili wa Hazina** na **Ofisi ya Rais Utumishi**.

Tunatambua uwekezaji wenu kwa maana ya **rasilimali fedha**, **rasilimali watu**, **miongozo na maelekezo** ambayvo vinatuwezesha kutekeleza majukumu yetu.

Nikushukuru tena wewe binafsi Mgeni Rasmi, kwa ukaribu wako kila tunapokuhitaji, na kwa kuwa nasi siku ya leo ya kuelimishana masuala mengi ndani ya Tasnia ya Afya ya Mimea.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza.**